


MWANANCHI

Ndani

ya habari

RAIS WA ZAMANI WA BOTSWANA AMNADI
MGOMBEA WA PINZANI UK 28 >



Elias Msuya, Mwananchi
emsuya@mwananchi.co.tz

Oktoba 10 ya kila mwaka dunia huadhimisha Siku ya Kimataifa ya Afya ya Akili. Siku hiyo huadhimishwa ili kuongeza ufahamu wa suala hilo.

Khamis Juma (si jina lake halisi) aliyejewa mfanyakibashara wa mazao ya kilimo mkoani Mwanza, ameathirika na ugonjwa wa akili. Kwa sasa anaishi katika kituo cha kurekebisha afya ya akili kilichopo eneo la Vikuruti wilayani Temeke, Dar es Salaam.

Kituo hicho kinamilikiwa na Hospitali ya Taifa ya Muimbili (MNH).

Akizungumza hivi hivi karibuni wakatti Shirika la Kuchota Busara za Wazee Wanawake (TEWWY) lilipowatembelea, Juma, ambaye sasa afya yake imeimarika, anasema anatamani kufungua duka la rejareja kama njia ya kutafuta maisha baada ya kuruhusiwa kutoka kituoni hapo.

"Nilikuja Dar es Salaam nikitoka Mwanz. Nilikuja kufanya biashara. Lakini nilianza kuumwa kiasi cha kupo-teza fahamu," anasema Juma.

"Niliambiwa na ndugu zangu baadaye kuwa polisi waliniokota nikiwa maeneo ya Kariakoo na kumipeleka Hospitali ya Taifa ya Muimbili ambako nilipelekwa wodi ya wagonjwa wa akili, nilikopatiwa matibabu.

"Baada ya kupata nafuu, waliniuliza kama naweza kuletwa kituo hiki na niliwakubalia. Hapa tumekuwa tukijifunza stadi za kazi kama kulima bustani na kufuga ng'ombe na kuku, huku tukutimia dawa."

INAENDELEA UK 26



KUANDAA MAISHA YA WAGONJWA WA AKILI BAADA YA MATIBABU